# BARAZA LA HABARI TANZANIA

S.L.P 10160, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2775728 / 2771947
Simu ya mkononi: +255 719 494640
+255 767 494826 / 784 314880
Nukushi:+255 22 2700370
Barua pepe: media@mct.or.tz
Tovuti: http://www.mct.or.tz
S.L.P 3490, Zanzibar
Simu: +255 24 2239728,

P.O. Box 10160, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 2775728 / 2771947
Mob: +255 719 494640 / 686 494640
+255 767 494826 / 784 314880
Fax:+255 22 2700370
E-mail: media@mct.or.tz
Website: http://www.mct.or.tz
P.O. Box 3490, Zanzibar
Tel: +255 24 2239728


## Tamko la Wadau wa Habari Kuhusu Azma ya Serikali Kupeleka Miswada ya Haki ya Kupata Habari na Huduma za Vyombo vya Habari kwa Utaratibu wa Hati ya Dharura

Sisi wadau wa masuala ya habari na upatikanaji wa taarifa tumepokea taarifa za utayari wa miswada muhimu miwili ya Haki ya Kupata Habari (Access to Information Bill) na Huduma za Vyombo vya Habari (Media Services Bill) kwa faraja. Miswada hii imekuwa ikisubiriwa kwa muda mrefu tangu wadau na wananchi walipoaanza kuidai ili kusaidia upatikanaji wa taarifa na habari kwa ajili ya maendeleo ya taifa lote kwa ujumla pamoja na kuboresha uendeshaji wa vyombo vya habari.

Tangu muswada ulipotolewa na serikali kwa mara ya kwanza mwezi Oktoba mwaka 2006 na kuondolewa, wadau na wananchi wamekuwa wakitazamia kuwa miswada miwili iliyoboreshwa kutokana na maoni na mapendekezo yao ingewasilishwa bungeni mapema zaidi.

Maoni na mapendekezo ya wadau wa habari juu ya muswada wa Haki ya Kupata Habari wa mwaka 2006 yalikamilika na kuwasilishwa serikalini mwaka 2007, na mapendekezo ya muswada wa Huduma za Vyombo vya Habari mwaka 2008. Ni faraja kwa wadau kwamba serikali imeona mantiki ya kuandaa miswada miwili tofauti ya Haki ya Kupata Habari na Huduma za Vyombo vya Habari.

Ni wazi kuwa, kuwasilishwa kwa miswada hii kunaendana na dhamira iliyooneshwa na serikali katika mipango na ahadi zake mbalimbali katika uendeshaji wa shughuli za serikali kwa uwazi. Aidha, miswada hii inaendana na dira ya kuimarisha demokrasia, uwajibikaji na utawala bora pamoja na ushirikishwaji wa wananchi na kuheshimu haki za binaadamu.

Kwa maoni yetu, kukamilika kwa miswada hii, kunatimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais Dk. Jakaya Mrisho Kikwete na serikali kwamba sheria hizo zingetungwa kabla ya kumalizika kwa serikali ya awamu ya nne ya utawala wa nchi yetu. Kutungwa kwa sheria za Haki ya Kupata Habari ni moja ya dhamira za mipango ya kuendesha



*For a strong and ethical media that contributes towards a more democratic and just society*

shughuli za serikali kwa uwazi kama vile APRM, OGP, UPR na EITI.[1] Katika mkutano wa kimataifa wa OGP uliofanyika jijini London mwaka 2013 na 2014 Rais alirudia ahadi kuwa sheria za Haki ya Kupata Habari zitatungwa April 2014. Hatua hii inaondoa taswira ya kwamba serikali haikuwa na dhamira ya kuhakikisha kwamba sheria hizi zinapatikana.

Hata hivyo, tukiwa wadau muhimu tuliolifanyia kazi suala hili la kupatikana kwa sheria ya Haki ya Kupata Habari na Huduma za Vyombo vya Habari kwa takriban muongo mmoja, tumeshangazwa sana na usiri mkubwa uliotanda mchakato wa kupelekwa miswada hii bungeni. Tulitarajia kuwa mchakato wa kutunga sheria hizi mbili ungefanyika kwa uwazi wa hali ya juu.

Kinyume chake, wadau wamepata taarifa kwa ghafla kupitia ratiba ya mkutano wa 19 wa Bunge la Tanzania pasipo kujulishwa wala kushirikishwa katika hatua za mwisho za matayarisho ya miswada yenyewe.

Tulitazamia kuwa miswada hii ingepelekwa bungeni kwa utaratibu wa kawaida ambapo muswada husomwa mara ya kwanza kabla ya wadau kuujadili na kutoa maoni ambayo huingizwa katika muswada kabla ya kusomwa mara ya pili na kupitishwa. Aidha, taarifa ya kupelekwa kwa muswada hupaswa kutolewa angalau siku 21 kabla ya muswada kusomwa bungeni.

Kwa mantiki hiyo, pamoja na uhitaji wa muda mrefu wa sheria hizi, tunaona kuwa ni jambo la msingi utaratibu wa kawaida wa kuwasilisha miswada ufuatwe. Miswada hii haistahili kupelekwa kwa hati ya dharura hasa ikizingatiwa kuwa haki ya kupata habari ni **haki wezeshi** ambayo mtu akiikosa yuko hatarini kukosa haki nyingine nyingi.

Tunaona kuwa kuwasilishwa miswada hii kwa hati ya dharura kunaondoa fursa ya wadau na wananchi kushiriki kikamilifu katika utungaji wa sheria hizi za msingi, kama inavyotakiwa katika Ibara ya 21 (2) ya katiba ya Tanzania.

Kwa hiyo wadau tunatoa wito:

---


[1] APRM ni mpango wa umoja wa Afrika (AU) wa nchi wanachama kujipima katika maeneo yanayohusiana na uwazi na uwajibikaji serikalini. OGP ni mpango wa kimataifa wa kuhamasisha uendeshaji wa shughuli za serikali kwa uwazi. EITI ni mpango wa kuboresha uwazi katika sekta za uziduaji kama vile uchimbaji wa madini na gesi. UPR ni mpango wa umoja wa mataifa wa kuzipima nchi katika kiwango cha utekelezaji wa haki za binaadamu hususan haki ya kupata habari. Tanzania ni mwanachama na inatekeleza mipango hiyo yote.

1. Kwa serikali kusitisha uwasilishwaji wa miswada hii miwili kwa utaratibu wa hati ya dharura ili kuwapa fursa wadau na wananchi kuipata miswada hiyo, kuisoma,kuichambua na kutoa maoni yao. Serikali itumie mkutano wa 19 wa Bunge la Tanzania kusoma miswada hii kwa mara ya kwanza kama hatua ya kuitayarisha kupokea maoni ya wadau kwa miezi inayokuja.
2. Kwa Bunge la Tanzania na uongozi wake kutokubali kupokea na kujadili miswada hii kwa utaratibu wa hati ya dharura.

Kwa kuwa haki ya kupata habari ni haki wezeshi, hakuna budi kuhakikisha kuwa unakuwepo ushiriki mpana wa wananchi katika hatua zote za utungaji wa sheria hizi mbili. Serikali inapaswa kuwezesha upatikanaji wa nakala za kutosha za miswada hii kwa umma, na kutoa muda wa kutosha kwa wananchi kuchangia maoni yao kikamilifu. Ili kuwezesha hilo, tuko tayari kuhamasisha utoaji wa maoni juu ya miswada hii.

**Hitimisho**

Tunatarajia serikali itaona umuhimu wa hoja na mapendekezo yetu. Miswada ya Haki ya Kupata Habari na Huduma za Vyombo vya Habari isiharakishwe na kuwasilishwa kwa hati ya dharura. Badala yake serikali ifuate taratibu wa kawaida wa uwasilishwaji na upitishaji wa miswada bungeni. Tunatarajia na kutegemea kuwa Bunge litafanya kazi yake ya kuishauri serikali kufuata utaratibu mzuri zaidi wa uwasilishaji wa miswada hii na kuchangia miswada hiyo kwa kuzingatia maslahi mapana ya kitaifa wakati muafaka utakapofika.



*Kajubi D. Mukajanga*
**Katibu Mtendaji Baraza la Habari Tanzania na Mwenyekiti wa Umoja wa Wadau wa Habari**

**Machi 20, 2015**

**Wadau**:

1. Media Council of Tanzania (MCT)

2. Sahara Media Group
3. Policy Forum
4. Legal and Human Rights Centre (LHRC)
5. The Guardian Limited
6. Mwananchi Communications Ltd (MCL)
7. Twaweza
8. Tanzania Media Fund
9. Free Media Ltd
10. Tanzania Citizens' Information Bureau (TCIB)
11. Sikika
12. Hali Halisi Publishers
13. Tanzania Media Women's Association (TAMWA)
14. Tanganyika Law Society (TLS)
15. National Organizational for Legal Assistance (nola)
16. Tanzania Editors Forum (TEF)